
WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA SIKU 10 KUANZIA TAREHE 12 HADI 22 FEBRUARI, 2026







**Imeandaliwa na;**

**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**


P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania
Phone: 0800114031 / 0800114032
E-mail: barua@wrbwb.go.tz
Website: www.wrbwb.go.tz

**Februari, 2026**

Yaliyomo

1. UTANGULIZI
2. ATHARI
3. UTABIRI WA HALI YA MAJI
4. USHAURI
5. HITIMISHO

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika Catchment (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 22 Februari, 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo. waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).




Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu


### 1.1 ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA

Uwezekano wa kiasi cha maji kuwa chini ya mahitaji (demand), hali inaweza kusababisha upungufu wa maji ikilinganishwa na mahitaji ya sekta mbalimbali.

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 12 hadi 22 Februari, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.**

| **Jina la Mto** | **Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji** | **Kielelezo** |
|---|---|---|
| Ruvu | Utabiri unaonyesha wingi wa maji utaongezeka na kuwa juu ya wastani wa muda mrefu (2009-2024) kuanzia tarehe 21 Feb,2026 kutokana na uwezekano wa kuwepo na mvua katika safu ya Milima ya Uluguru. Aidha, kiwango cha maji kilichopo kwa sasa na siku kumi zijazo ni himilivu na kinatosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali ikiwemo mahitaji ya maji majumbani katika Mitambo ya DAWASA ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Mahitaji uwandani ni mita za ujazo sita (6) kwa sekunde (**jendwali Na.1)**. |  |

## 3. USHAURI KWA SEKTA MBALIMBALI

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Mifugo, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuchukua tahadhari dhidi ya upungufu wa maji unaoweza kujitokeza kwa kutumia maji yalipo kwa ufanisi na kuthibiti upotevu wa maji. Aidha Bodi inazishauri sekta hizi kuwa na njia mbadala ya upatikanaji wa maji ikiwemo visima virefu endapo kutatokea upungufu wa maji katika Mto Ruvu.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha wanufaika na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.